



HOTUBA YA MSWADA WA SHERIA YA KUIDHINISHA MAKISIO YA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

- 1. Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, tukiwemo sisi waja wake. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku, neema kubwa na ndogo kwa kutujaalia sote uzima na uwezo wa kukutana tukiwa katika hali njema ya afya na amani ambayo inatuwezesha kuendesha shughuli zetu kwa utulivu, maelewano na upendo kwa maslahi ya nchi yetu, pia napenda nikushukuru wewe kwa dhati kabisa na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa ambayo yametuwezesha sisi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuweza kukamilisha jukumu tulilopewa la kuwasilisha Mswada wa Makadirio wa Matumizi kwa bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024.
- 2. Mheshimiwa Spika,** Napenda nitumie fursa hii kwa mara nyengine tena, kuwasilisha Mswada huu kwa ajili ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kutimiza wajibu wa Kikatiba chini ya kifungu cha (106), ambacho Waziri mwenye dhamana



ya Fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi kila mwaka wa fedha unapoanza, Kwa heshima kubwa, na ruhusa yako naomba sasa niwasilishe Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nane na Arubaini, Millioni Mia Nane na Hamsini na Tatu, Laki Saba na Thalathini na Mbili Eflu (TZS 2,840,853,732,000)** kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mpaka kufikia mwaka wa fedha unoishia siku ya tarehe 30 Juni 2023/2024 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

3. **Mheshimiwa Spika**, Kuidhinishwa kwa bajeti za Wizara na Taasisi zote za Serikali kunapelekea Mswada wa Makisio na Matumizi kutoa uwezo kwa Serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tatu na Nane, Million Hamsini na Sita **(TZS 1,308,056.0)** kutumika kwa ajili ya kazi za Kawaida na Shilingi Trilioni Moja, Billion Mia Tano Kumi na Nne, Million Mia Saba na Tisini na Saba na Laki Saba **(TZS 1,514,797.7)**, kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, na Shilingi Bilioni Kumi na Nane **(TZS 18,000.0)** kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
4. **Mheshimiwa Spika**, Kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha Serikali kukopa fedha Ndani na Nje,



kwa ajili ya matumizi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2024. Kiasi cha fedha kilichoainishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya Kifungu cha 5(1) cha Mswada huu.

5. **Mheshimiwa Spika**, Mswada huu una jumla ya vifungu **Nane**: Kifungu cha **kwanza** kinazungumzia **Jina fupi**. Kifungu cha **pili** kinazungumzia **Tafsiri**. Kifungu cha **tatu** kinazungumzia **Utoaji wa Shilingi 2,840,853,732,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali**.
6. **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha **nne** chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia **Uwezo wa Waziri Kukopa**, Kifungu cha **tano** chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia **Uwezo wa Waziri kwa Maombi ya ziada**, kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura au pale haja itakapotokezea.
7. **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha **sita** kinazungumzia **Marejesho ya Mkopo na Riba**. Kifungu cha **saba**, chenye vifungu vidogo viwili kinazungumzia Kukubaliwa kwa **Fedha zilizopitishwa kwa Matumizi ya Kazi za Kawaida na Miradi ya Maendeleo** Kifungu cha **nane** ambacho ni cha



mwisho kinazungumzia, **Mfuko wa Pamoja wa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.**

8. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo haya mafupi ya Mswada huo, kwa dhati naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kuujadili na hatimaye kuupitisha Mswada huu, ili uwe ni Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha **2023/2024.**

9. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.